

Kuza Biashara Yako Kupitia Programu Ya ENGINE

Mpango wa eCoupon kwa kupitia programu ya ENGINE unaisaidia biashara yako kupata punguzo la bei zilizopo katika baadhi ya huduma za mafunzo na ushauri wa kibiashara

Programu ya kuwezesha ukuaji kupitia uwekezaji na biashara (ENGINE), inasaidia watoa huduma za mafunzo na ushauri wa kibiashara walioidhinishwa na ENGINE kutoa punguzo la hadi 40% kutoka kwenye bei ya soko kwa baadhi ya huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara kama: usimamizi wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu, mpango biashara, huduma za fedha (mikopo), huduma ya kurasmisha biashara, masoko na kutangaza biashara.

Inavyofanya Kazi



NENDA KWA MTOA HUDUMA

Omba huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara kutokana na taratibu za mtoa huduma. Mtoa huduma atakupata bei ya huduma husika ambayo itaonyesha punguzo la bei linalopatikana kutokana na mpango wa ENGINE, kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini.



JAZA FOMU

Kamilisha kujaza fomu ya maombi ya punguzo la bei na umkabidhi mtoa huduma. Hii itahusisha pia kujaza namba yako ya simu ya mkononi ambayo itatumika kwa mawasiliano, baada ya hapo, mtoa huduma atakutaarifu kama umekidhi vigezo vya kupata punguzo la bei kutoka katika programu ya ENGINE.



POKEA KUPONI KUPITIA SIMU YAKO

Kama umekidhi vigezo, utapokea ujumbe mfupi kupitia kwenye simu yako ya mkononi, utakaonyesha namba ya kuponi ya punguzo la bei kutoka katika programu ya ENGINE.



LIPIA

Unapolipia huduma ya ushauri au mafunzo ya kibiashara, muonyeshe mtoa huduma namba ya kuponi uliyopata kwenye ujumbe wa simu yako ili kuomba punguzo na ulipe kiasi kilichobaki cha bei ya huduma kwa fedha taslim, hundi, MPesa/Tigo Pesa/Airtel money n.k. Hapo utakuwa umekamilisha taratibu zote.

JEDWALI LA PUNGUZO ZA BEI

Mpango wa punguzo	Bei kutoka (Tsh)	Bei hadi (Tsh)	Punguzo (Tsh)
	A	B	C
1	250,000	500,000	100,000
2	501,000	750,000	200,400
3	751,000	1,000,000	300,400
4	1,250,000	1,500,000	500,000
5	1,501,000	1,750,000	600,400
6	1,751,000	2,000,000	700,400
7	2,001,000	2,500,000	400,200
8	2,501,000	3,000,000	500,200
9	3,001,000	3,500,000	600,200
10	3,501,000	4,000,000	700,200
11	4,001,000	4,500,000	800,200
12	4,501,000	5,000,000	900,200

"Feed the Future" ni mpango toka serikali ya Marekani kuthibiti njaa duniani. Ikiwalenga wakulima wadogo wadogo, hasa wanawake, "Feed the Future" inasaidia nchi washirika kuendeleza sekta za kilimo ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi

na biashara, kuongeza kipato na kupunguza njaa, umaskini na utapiamlo. USAID ni wakala wa serikali ya Marekani anayeongoza kufanya kazi ya kukomesha umaskini uliokithiri duniani na kuwezesha ustahimilivu na demokrasia katika jamii ili zitambue uwezo wao.